

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI C

S.I

SUMBAWA

TAREHE.....

MOBILE,0744 1

07542

KUMB/CH/JI/VOL1

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH;MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHALA WILAYA YA NKASI  
MKOA WA RUKWA MWAKA 20.....

**1.UTANGULIZI**

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya CHALA, ipo ka Halmashauri ya wilaya ya Nkasi.Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe .....unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe.....na mwisho wa kuripoti ni tarehe.....[ndani ya siku saba]

2.Mambo muhimu ya kuzingatia

**A.SARE ZA SHULE KWA WAVULANA**

- i. Sare ya shule hii ni suruali mbili moja rangi ya kijani na nyingine rangi ya damu ya mzee
- ii. Shati nyeupe mbili mikono mifupi
- iii. Sweta mbili moja rangi ya kijani na lingine rangi ya damu ya mzee
- iv. Tai mbili ya kijani na nyingine damu ya mzee
- v. Kiatu cheusi cha kamba
- vi. Daftari tisa [9]kubwa
- vii. Soksi nyeusi jozi mbili ziwe ndefu.

**B.SARE ZA SHULE KWA WASICHANA**

- i. Sketi mbili ndefu za kufunika soksi zake moja rangi ya kijani na nyingine damu ya mzee
- ii. Sweta mbili moja rangi ya kijani na nyingine damu ya mzee
- iii. Tai mbili moja rangi ya kijani na nyingine damu ya mzee
- iv. Shati nyeupe mbili mikono mifupi
- v. Soksi jozi mbili nyeupe ziwe ndefu
- vi. Daftari tisa [9]kubwa
- vii. Viatu vyeusi vya kamba

C.Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule

**3.MAHITAJI YA HOSTELI KWA WASICHANA**

- i. Mahindi dede nane[8] kwa mwaka
- ii. Ma harage debe tatu[3]kwa mwaka
- iii. Pesa kiasi cha tTsh 60,000/=kwa mwaka;mchanganuo,kumlipa mpishi,kununua chumvi,mafuta ya kupikia,kuni kusaga mahindi.
- iv. Shuka mbili moja ya pink na nyingine blue bahari
- v. Godoro ft mbili na nusu
- vi. Ndoo ndogo ya kuogea,kikombe,kijiko na sahani

#### 4. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni [preparation]
- iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule
- vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- ix. Kutunza mali za umma

#### 5. MAKOSA/MAMBO YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- i. Wizi
- ii. Uasherati na ushoga
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungu, kubeli na kadhalika
- v. Kupiga au kupigana
- vi. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
- vii. Kudharau bendera ya Taifa
- viii. Kuwa mjamzito/kupata mimba
- ix. Kusababisha mimba
- x. Kutoa mimba
- xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xiii. Kuwa na simu ya mkononi

#### 6. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI

##### NA MWANAFUNZI

- i. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospital ya serikali, Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni
- ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
- iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

#### 7. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO /MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU

...*Fatma Mubara*...

FATMA MUBARAKA

MKUU WA SHULE

